BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Tano – Tarehe 05 Mei, 2022
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka 2022/2023.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa Mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

62. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Kumekuwa na malalamiko dhidi ya wafanyakazi kutowajali wananchi wanapohitaji huduma mbali mbali maofisini.

    (a) Je, ni lini Serikali itatoa muongozo maalum kwa zile taasisi zinazotoa huduma moja kwa moja kwa wateja pamoja na kupatiwa mafunzo maalum ya kumjali mteja

(*Customer Care*) kwa wafanyakazi hao.

(b) Je, ni malalamiko mangapi na ya aina gani Serikali imepokea kutoka kwa wananchi walionyanyaswa kwa mwaka 2021/2022.

<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>

9. MHESHIMIWA BIHINDI HAMAD KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Wananchi wa Zanzibar wanaendelea kujenga matumaini kwa Serikali yao inayoongozwa kupitia Ilani ya CCM kwa kujenga mahusiano mema na mataifa mbali mbali na kupelekea upatikanaji wa fedha za ahuweni za Covid 19 na kuwapatia fursa za mikopo wajasiriamali.

(a) Je, ni vigezo gani Serikali inavitumia na vinawezesha kikundi kupatiwa fedha hizo za mkopo.

(b) Je, ni gharama ya kiasi gani za awali zinazotumika kukamilisha masharti hayo hasa kwa wanavikundi waliopo maeneo ya vijijini.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

53. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Mji wa Chake Chake ni miongoni mwa miji iliyokuwa na harakati mbali mbali za kijamii na za Serikali, hata hivyo kumekuwa na changamoto ya uhaba wa sehemu za maegezo ya vyombo vya moto jambo ambalo linapelekea usumbufu mkubwa kwa wananchi.

(a) Je, ni lini Serikali itafikiria kuwa na eneo maalum la maegesho la kisasa la gari (car and lorry parking) katika mji wa Chake Chake.

(b) Je, ni lini Serikali itaamua kubadilisha moja kati ya viwanja vya michezo kuwa eneo jipya la maegesho ya kisasa.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

36. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kuna tafauti ya viwango vya kodi kati ya wafanyabiashara.

(a) Je, ni kigezo gani kinachotumiwa na Mamlaka ya Kukusanya Mapato inapopanga viwango vya kodi kwa wafanyabiashara.

(b) Je, ni sawa kwa wafanyabiashara wakubwa ambao wanalipa kodi kwa asilimia 15% kuingia kwenye ushindani na wafanyabiashara wadogo wanaolipa kodi kwa asilimia 3% ili kupata zabuni za kuiuzia bidhaa Serikali.

(c) Kwa nini kusiwe na kiwango sawa sawa kwa sababu mara nyingi wenye kulipa kodi za chini zabuni zao zinakuwa za gharama ya chini.

Wizara ya Afya:

10. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Katika Shehia ya Ukutini zipo nyumba za daktari, lakini kwa muda mrefu sasa inatumika nyumba moja tu.

(a) Je, ni sababu gani zinazopelekea kukosa daktari wa kuishi.

(b) Je, Wizara imejipanga vipi kumpeleka daktari ambaye ataishi katika nyumba hiyo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

15. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika kipindi cha miezi ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la ajali kwa wenye vyombo vya maringi mawili pamoja na watembea kwa miguu, hali ambayo husababisha vifo na ulemavu wa kudumu na kurudisha nyuma juhudi za Serikali katika kuwapatia wananchi maendeleo.

(a) Je, Wizara yako inaweza kuwafahamisha wananchi, ni sababu zipi zinazopelekea ajali hizo.

(b) Kwa muda mrefu sasa alama nyingi za barabarani kwenye maeneo ya kuvukia watu "zebra cross" zimefutika na kusababisha hatari kwa wenda kwa miguu. Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba alama hizo zinakuwepo wakati wote.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

69. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kwa kuendelea kuwatunza wazee wasiojiweza katika nyumba za Sebleni na Welezo. Hata hivyo, hivi karibuni wazee hao wamekuwa wakipambana na vitendo mbali mbali vya kihalifu kama wizi pamoja na kuhatarishiwa maisha yao.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulimaliza tatizo hili.

(b) Je, ni huduma gani Serikali huwa inatoa kwa wazee hao.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

7. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya juhudi kubwa ya kuhakikisha tatizo la upatikanaji wa huduma za maji nchini linaondoka. Pamoja na juhudi hizo zinazostahiki kupongezwa, bado maeneo ya Mjini yanapata changamoto ya uhaba wa maji.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuimarisha miundombinu chakavu na kuweka mipya ili kuondoa tatizo hilo.

(b) Je, mipango hiyo inategemewa kuchukuwa muda gani kukamilika.

<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

21. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Makongeni ni miongoni mwa skuli iliyofanya vibaya katika matokeo ya kidato cha nne kwa mwaka 2021 na kwa kuwa Serikali imeshatoa kibali cha kuajiri walimu wapya.

Je, ni walimu wangapi wa sayansi na sanaa watakaoajiriwa kwa mwaka 2022/2023.

39. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Serikali yetu inahimiza suala la usafi wa miji na vijiji vyetu. Kumejitokeza utaratibu wa kufanya usafi kila baada ya muda chini ya usimamizi wa taasisi husika.

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea kwa watumishi wa umma hususan walimu, kufanya usafi katika maeneo ambayo si maeneo yao ya kazi.

(b) Kwa kuwa mara nyingi usafi hufanyika siku za mapumziko je, hatuoni kuwa tunaenda kinyume na Sheria za Utumishi kwa kuwataka walimu kufanya usafi siku za mapumziko.

(c) Ikiwa suala la usafi ni la kijamii au la wafanyakazi, ni kwa nini watakiwe walimu tu kushiriki katika usafi kinyume na wafanyakazi wa taasisi nyengine mfano Afya, Mahakama, Kilimo nyenginezo.

III. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

<u>Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar, (Raya Issa Msellem)
05 Mei, 2022. KATIBU WA BARAZA